

JAMHURI YA RWANDA



WAZIRA WA AFYA  
P.O. BOX 84 KIGALI  
[www.moh.gov.rw](http://www.moh.gov.rw)

**Hatua za kuzuia na kupambana COVID-19 zinaohusu Madereva wa Malori wanaofanya safari ndani na nje ya nchi kwa lengo za Biashara ya Mpakani - 16 Septemba 2020**

Tukiangalia mwenendo wa sasa ugonjwa wa COVID-19 nchini Rwanda na hasa kwenye madereva wa malori wanaosafiri ndani na nje ya nchi.

Wizara ya Afya imefanya tathmini ya hatua zilizopo za kuzuia na kupambana na ugonjwa wa COVID-19 haswa upande wa madereva wa malori na kusasisha miongozo ifuatayo ili kuhakikisha usafirishaji rahisi wa bidhaa na kuendelea kuzingatia usalama:

1. Malori yote yanayobeba bidhaa zinazoharibika, bidhaa za petroli, lori za mizigo ya bidhaa hatari, dawa na bidhaa za matibabu kuitia Rwanda na zile zinazopita nchini Rwanda hazitasindikizwa tena lakini zitafutiliwa kwa mbali kwa kutumia zana ya ufuatiliaji wa mizigo ya elektroniki / GPS (Global Positioning System). Kwa hivyo, Madereva watapewa kifaa cha elektroniki na ni marufuku kupindua au kuharibu kifaa hicho. Madereva wanatikiwa kukirudisha kifaa hicho kwenye vituo vya mpaka baada ya safari.
2. Zowezi la kupima dalili za COVID-19 litaendelea mpakani kwa madereva wote wanaovuka na kwingia nchini Rwanda. Madereva watakaokutwa na dalili za ugonjwa watatibiwa kulingana na miongozo iliyopo ya kiafya inayopatikana katika ([www.rbc.gov.rw](http://www.rbc.gov.rw))
3. Vipimo vya COVID-19 vitakuchukuliwa mara kwa mara ili kujua kiwango cha ugonjwa huo kwenye madereva wa malori.
4. Madereva wote wa malori wanaombwa kufuata kanuni za kuzuia mambukizi ya COVID-19 (kuvaaa barakoa, kukaa mbali na watu wengine, kuzingatia usafi wa mikono na kuepuka kusalimiana kwa kupeana mikono).

5. Madereva wa malori wanaohusika wanaruhusiwa kusimama tu katika vituo maalum na kulala kwenye maeneo yalijotengwa kwa ajili yao.
6. Polisi ya Rwanda itaendelea kusaidia utekelezaji wa miongozo ya kujikinga kutoka mpakani mpaka mahali pa kupakua mizigo.
7. Hatua hizi zitatekelezwa na taasisi zote zinazohusika katika vituo vyta mipaka na katika barabara nchini.
8. Hatua hizi zitatekelzwa mara tu baada ya kutiwa saini. Kuepuka au kutotii hatua hizi kutasababisha adhabu kali kulingana na sheria za nchi. Tungependa kuwakumbushe tena kwamba madereva watalipa upimaji wa COVID-19.
9. Hatua hizi zimebadilishwa kufuatia hali ya sasa ya magonjwa ya COVID-19 na zinaweza kuboreshwa tena kufuatana na hali ya afya na tathmini ya kawaida.

Kwa maelezo zaidi au usaidizi, tafadhali piga simu kwa nambari zifuatazo:

**Afya:** 114 au +250 789 198 119

**Polisi:** 112 au +250 788 31 10 02, +250 788 31 18 54

21 SEPT 2020

Tangazo limotolewa leo tarehe.....

